


# KIJARIDA CHA KUJIELIMISHA JAMII JUU YA MASUALA MUHIMU YA HAKI ZA ARDHI KUHUSU UANDAaji WA MPANGO WA MATUMIZI YA ARDHI YA KIJAJI



## Utangulizi

Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Na.6 ya mwaka 2007 ni zao mojawapo la sheria za ardhi za mwaka 1999 ambazo zinatilia mkazo mgawanyo wa ardhi katika makundi mbalimbali ili kukidhi matakwa na maslahi ya watumiaji wake. Sheria hii imeweka misingi ya upangaji na utumiaji wa ardhi inayozingatia sera ya taifa ya ardhi ya mwaka 1995 pamoja na sera ya maendeleo ya makazi ya taifa ya mwaka 2000. Baadhi ya misingi hiyo ni kama ifuatayo;

- Kuwezesha upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya makazi na maendeleo kwa makundi yote ya jamii wakiwemo wanawake, vijana, wazee, walemavu, wafugaji n.k
- Kuboresha miundo mbinu na huduma za jamii kwa maendeleo ya watu
- Kupanua wigo wa ajira na kupunguza hali ya umaskini katika jamii
- Kuwezesha mfumo utakaoruhusu mashirika yasiyo ya kiserikali kushiriki katika mipango ya matumizi ya ardhi
- Kulinda makazi ya watu na rasilimali anuai dhidi ya uchafuzi wa mazingira kwa maendeleo bora ya jamii
- Kujenga uwezo wa kitaalamu katika utoaji wa mafunzo kwenye fani zinahusiana na mipango ya matumizi ya ardhi

## 3.1 Malengo na Faida za mipango ya matumizi ya ardhi

### 3.1.1 Malengo ya mipango ya matumizi ya Ardhi

Kusudio hasa la kutungwa kwa sheria ya mipango ya matumizi ya ardhi ni pamoja na kukidhi malengo yafuatayo.

- Kuwezesha usimamizi wenye ufanisi wa matumizi ya ardhi
- Kuwezesha wamiliki na watumiaji wa ardhi kuzingatia matumizi bora ya ardhi na uzalishaji wenye tija kwenye ardhi wanayomiliki
- Kuwezesha uhakika na usawa katika kupata rasilimali za ardhi
- Kuwezesha matumizi endelevu ya ardhi
- Kuwezesha uanzishwaji wa mifumo ya kukabiliana na migogoro ya matumizi ya ardhi
- Kuweka mfumo wa kuratibu ujumuishaji wa kissekta katika ngazi mbalimbali ikiwemo miundo ya kisiasa na kiutawala
- Kuweka mfumo wa kuhuisa misingi ya maendeleo ya taifa iliyoainishwa katika sera za Serikali

### 3.1.2 Faida za mipango ya matumizi ya ardhi

Mpango wa matumizi ya ardhi una faida nyingi kwa jamii husika na kwa matumizi endelevu ya rasilimali ardhi na rasilimali zilizomo ardhi kwa vizazi vya sasa na vya baadae. Baadhi ya faida za mpango wa matumizi ya ardhi ni pamoja na:

- Kuondoa migogoro ya ardhi baina ya watumiaji wa ardhi.
- Kusaidia utunzaji wa ardhi na hasa vyanzo vya maji.
- Kuzuia ufekaji wa misitu na mapori yaliyohifadhiwa kwa matumizi maalum.
- Kuwezesha matumizi endelevu ya ardhi na rasilimali zake kutokana na kupangilia matumizi ya rasilimali hizo kulingana na mahitaji ya makundi mbalimbali ya kijamii na kuepusha mwingiliano wa kimatumizi baina ya makundi.

### 3.1.3 Athari za kukosekana kwa mipango ya matumizi ya ardhi

Bila shaka kuna athari nyingi za kutumia ardhi kiholela yaani bila kufuata mpangilio au utaratibu maalumu uliowekwa kwa misingi ya kitaalamu. Ingawa si rahisi kuainisha kila athari katika sehemu hii baadhi yake ni kama zifuatazo;

- Kuongezeka kwa idadi ya migogoro miongoni mwa watumiaji wa ardhi.
- Kutokuwa na uhakika wa miliki na matumizi ya ardhi. Hii natokana na ukweli kuwa kila mtumiaji wa ardhi hujiona kuwa ana haki ya ujumla ya eneo au ardhi husika wakati ikipangiliwa matumizi yake huenda hata haimhusu yeye bali watu wengine
- Maendeleo duni ya soko la ardhi lisilo rasmi
- Uharibifu wa udongo na vyanzo vya maji
- Ufeykaji misitu na mapori

## 3.2 Mamlaka za upangaji na usimamizi wa mipango ya matumizi ya Ardhi

Sheria ya mipango ya matumizi ya ardhi inaunda vyombo mbalimbali vyenye mamlaka katika utayarishaji, usimamizi na utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi katika ngazi mbalimbali. Vyombo hivyo ni pamoja na; Waziri mwenye dhamana ya ardhi, tume ya taifa ya mipango ya matumizi ya ardhi, Halmashauri ya Wilaya na halmashauri ya kijiji. Aidha, kulingana na mahitaji ya kimaeneo, mipango ya matumizi ya ardhi inaweza kuandaliwa katika ngazi ya kanda na hivyo kulazimu kuwa na mamlaka za kikanda za kuwezesha uandaaji wake.

### 3.2.1 Ngazi ya taifa

Katika ngazi ya taifa, kuna tume ya taifa ya matumizi ya ardhi. Tume hii huundwa na wawakilishi kutoka sekta mbalimbali za kijamii ambao huteuliwa na waziri mwenye dhamana ya ardhi na huongozwa na Mkurugenzi Mkuu wa tume. Majukumu ya msingi ya tume ya taifa ya matumizi ya ardhi ni pamoja na; kuandaa mpango wa kitaifa wa matumizi ya ardhi, kuandaa mipango kabambe ya kikanda ya matumizi ya ardhi na kuratibu, kusimamia na kutoa mwongozo wa uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi kitaifa.

### 3.2.2 Ngazi ya Wilaya

Katika ngazi hii, halmashauri ya wilaya inatajwa na sheria ya matumizi ya ardhi namba 6 ya 2007 fungu la 21 kuwa ndiyo yenye mamlaka ya upangaji wa matumizi ya ardhi ya wilaya. Jukumu hili kwa mujibu wa fungu hilo, hutekelezwa kupitia kama ya kudumu ya halmashauri ya wilaya inayohusika na ardhi na mazingira. Pamoja na majukumu mengine, halmashauri ya wilaya ina jukumu la kuunda timu ya matumizi ya ardhi ya Wilaya maarufu kama PLUM yenye wajumbe 6 hadi 8 kutoka miongoni mwa sekta zinazohusika na ardhi kama vile kilimo, mifugo, maliasili, ardhi na maendeleo ya jamii na kuziwezesha Halmashauri za vijiji kuunda Kamati ya Usimamizi wa Ardhi ya Kijiji. Kwa pamoja kamati hizi hufanya tathmini shirikishi ya kijiji, kuweka Mpango kazi wa jamii, na hatimaye kuandaa rasimu ya mpango wa matumizi ya ardhi ya kijiji.

### 3.2.3 Ngazi ya Kijiji

Katika ngazi hii mamlaka inayohusika na maandalizi ya mpango wa matumizi ya ardhi ya kijiji ni halmashauri ya Kijiji ambayo inaweza kufanya utekelezaji wake kupitia kamati ya usimamizi na matumizi ya ardhi ambayo undani wake utaeleza katika aya zinazofuata. Jambo la msingi katika ngazi hii ni kuzingatia kuwa, mpango wa matumizi ya ardhi ya kijiji ni matokeo ya mchakato shirikishi ambao bila kufuata hatua zinazotakiwa utakosa uhalali wake na hasa pale wananchi wanapokuwa hawakushiriki kikamilifu kama mwananchi mmoja mmoja au kupitia mikutano yao mkuu ya vijiji.

## 3.3 Uandaaji wa Mpango wa Matumizi ya Ardhi ya Kijiji

### 3.1.1 Maana ya mpango wa matumizi ya Ardhi wa Kijiji

Kwa mujibu wa mwongozo wa tume ya Taifa ya Mpango wa matumizi bora ya ardhi wa mwaka 2010, (uk.10), mpango wa matumizi ya ardhi unatafsiriwa kuwa ni: utaratibu wa kutathmini na kupendekeza namna mbalimbali za matumizi ya maliasili/rasilimali ili kuinua hali ya maisha ya wanakijiji na kuondoa umaskini. Mwongozo unakazia kuwa, utaratibu wa kupanga, kutekeleza na kuhusha matumizi ya ardhi unafaa zaidi iwapo utafanyika kwa njia ya ushirikishwaji, ikiwa na maana kuwa watumiaji wakubwa wa ardhi ambao ni wanakijiji wanashirikishwa kikamilifu. Ili kuhakikisha kuwa wanakijiji wanashiriki kikamilifu, ni muhimu kuzingatia makundi mbalimbali yaliyopo katika kijiji (k.v. wakulima, wafugaji pamoja na jinsia na rika), ambayo yanaweza kuwa na utashi na malengo yanayotofautiana.

### 3.3.2 Hatua za uandaaji wa mpango wa matumizi ya ardhi Kijijini

Hatua ya kwanza. Maandalizi ya awali ngazi ya Wilaya Katika hatua hii Halmashauri ya Wilaya inapaswa kuunda kamati shirikishi ya mipango ya matumizi ya ardhi wilayani yenye wajumbe kati ya 6-8 kutoka katika idara zinazohusiana na ardhi kama vile ardhi, kilimo, mifugo, maliasili na maendeleo ya jamii. Timu ya wilaya ya PLUM itatakiwa kuandaa utaratibu wa utekelezaji wa mpango wa matumizi ya ardhi katika vijiji vilivyo kwenye halmashauri ya wilaya husika kulingana na rasilimali ilizo nazo ili kufanikisha uandaaji wa mipango ya vijiji kwa wakati.

Hivi sasa inaeleweka kuwa uhaba wa fedha ndilo tatizo la msingi linalokwamisha halmashauri nyingi za wilaya kutekeleza majukumu yake ya kuwezesha mipango ya matumizi ya ardhi katika himaya zake. Hata hivyo, inashauriwa kuwa ili halmashauri ziweze kumudu utekelezaji wa jukumu hili muhimu, ni vema zikaanza na baadhi ya vijiji badala ya kufikiria kutekeleza upangaji wa matumizi ya ardhi kwa vijiji vya wilaya nzima. Na hili linawezekana pia kwa kushirikiana na taasisi nyingine zenye miradi kama hiyo katika maeneo ya wilaya husika. Timu ya wilaya ikiwa na uhakika wa rasilimali fedha inapaswa kuandaa mpango kazi utakao iwezesha kutekeleza mipango ya wilaya nzima hatua kwa hatua.

### Hatua ya pili: Kufanya tathmini shirikishi ya matumizi ya ardhi ya kijiji.

Hatua hii inahusisha hatua ndogo nne. Hatua ya kwanza ni uhamasishaji wa wananchi katika vijiji vinavyoandaliwa mpango wa matumizi ya ardhi. Uhamasishaji huu hufanywa na timu ya wataalamu ya wilaya inayoitwa PLUM kwa ushirikiano na serikali ya kijiji na kamati ya matumizi ya ardhi ya kijiji. Baadhi ya

masuala yanayotakiwa kuwemo katika orodha ya uhamasishaji ni pamoja na madhumuni, umuhimu na utaratibu wa kutekeleza mpango wa matumizi ya ardhi, takwimu muhimu za kijiji kama vile idadi ya watu, kaya, mifugo na huduma za kijamii zilizopo kijijini pamoja na masuala ya msingi katika sera na sheria za ardhi. Hatua ndogo ya pili ni kufanya tathmini shirikishi ya kijiji ili kubaini idadi ya watu, mifugo, ukubwa wa eneo n.k. Tathmini hii hufanywa na halmashauri ya kijiji ikijumuika na kamati ya usimamizi wa matumizi ya ardhi ya kijiji kwa uwezeshaji wa timu ya PLUM. Ikumbukwe kuwa, tathmini shirikishi hufanyika kwa kukusanya, kuchambua na kuweka kumbukumbu takwimu zote muhimu za kijiji kwa kila kitongoji.

Hatua ndogo ya tatu; ni kuandaa mpango kazi wa jamii (community Action Plan). Mpango huu usichanganywe na mpango wa matumizi bora ya ardhi bali wenyewe ni kama ratiba ya namna utekelezaji wa mambo yaliyopangwa utakavyofanyika. Mpango kazi wa jamii huweka bayana mambo kama muda unaohitajika kufanya kila shughuli, kazi na majukumu ya watu binafasi na vikundi, uhusishwaji wa miradi ya kijiji na ya kitaifa na mambo yanayohitaji msaada kutoka nje ya kijiji husika. Hatua ndogo ya nne ni ujenzi na uimarishaji wa taasisi za kijiji kama vile halmashauri na mkutano mkuu wa kijiji pamoja na kamati zake kwa lengo la kuziwezesha kumudu majukumu yake katika uandaaji wa mpango wa matumizi ya ardhi kijijini. Taasisi hizi mbili zina umuhimu wa kipekee katika vijiji kwa mujibu wa sheria za ardhi na serikali za mitaa. Kwa mfano, kifungu cha 55 cha sheria ya serikali za mitaa kinaweka utaratibu wa kila kijiji kuwa na mkutano mkuu ambao kwa mujibu wa sheria ya ardhi ya vijiji namba 5 ya 1999 kifungu cha 8 ndio wenye mamlaka ya kuridhia au kukataa ugawaji wa ardhi ya kijiji unaopendekezwa na halmashauri ya kijiji.

### Hatua ya tatu: Kuweka Mipaka na matumizi ya Ardhi ya Kijiji

Kimsingi, ardhi ya Tanzania ni mali ya umma na imewekwa chini ya rais kama mdhamini kwaniaba ya wananchi wote. Ardhi hii imegawanyika katika matumizi kulingana na makundi yake yaani ardhi ya kawaida, ardhi ya hifadhi na ardhi ya kijiji. Hata hivyo, mipaka ya kundi lolote la ardhi inaweza kubadilika kutokana na mamlaka aliyo nayo Rais ya kuhawilisha yaani kubadili kundi au sehemu ya kundi moja la ardhi kuwa jingine. Hivyo basi baada ya hatua ya pili kukamilika, itakuwa imefahamika kuwa mipaka ya kijiji husika inatambulika na kubainishwa kwa vipimo vinavyotambulika. Hata hivyo, hatua hii ya tatu inaitaka timu ya PLUM ya Wilaya kuhakiki kupitia ofisi ya ardhi ya wilaya na kuweka ordha ya vijiji katika makundi yafuatayo:

- Vijiji ambavyo vimeshapimwa (vina ramani) na havina migogoro ya mipaka kisha kuviandaliwa cheti cha Ardhi ya Kijiji.
- Vijiji ambavyo mipaka yake inatambulika lakini havijapimwa na havina migogoro ya mipaka. Vijiji hivi vinaweza kuandaliwa ramani ya mipaka kwa njia ya chombo cha upimaji (GPS), na kuandaliwa Cheti cha Ardhi ya Kijiji
- Vijiji ambavyo mipaka yake ilishapimwa, lakini kwa sasa vina migogoro ya mipaka kwa mfano kama vimegawanyika. Migogoro ya mipaka itatuliwe kwanza, na kubaini mipaka inayokubalika kwa pande husika.
- Vijiji ambavyo havijapimwa na vina migogoro ya mipaka basi ni sharti kwanza migogoro hiyo itatuliwe kwanza, na kubaini mipaka inayokubalika kwa pande husika. Jukumu la msingi ili halmashauri ya Kijiji isimamie ardhi ya kijiji kwa mujibu wa wa sheria ni kutambua mipaka ya kijiji na kupata Cheti cha Ardhi ya Kijiji. Katika kufanya hili, Halmashauri ya Kijiji husika haina budi kuwasiliana na mamlaka za ardhi inayopakana na kijiji. Endapo kijiji kinapakana na hifadhi basi mamlaka ya hifadhi hiyo na endapo kinapakana na vijiji vingine basi Halmashauri za Vijiji hivyo, ili wakubaliane mipaka ya ardhi yao. Halmashauri ya Kijiji, aghalabu itakasimu shughuli hii kwa kamati: kama vile kamati ya kusimamia Matumizi ya Ardhi au Mazingira kwa kadri halmashauri itakavyoona inafaa.

### Cheti cha Ardhi ya Kijiji

Mara mipaka ya kijiji ikiishawekwa na kupimwa, mamlaka husika (Kamishna wa Ardhi) atatoa Cheti cha Ardhi ya Kijiji kwa Halmashauri

ya Kijiji kwa mujibu wa Fungu la 7 (6-12) la Sheria ya Ardhi Vijiji ya 1999. Hii ni hati muhimu inayopaswa kutunzwa na Halmashauri ya Kijiji, inayotumika kumaanisha mamlaka ya Halmashauri ya Kijiji kutawala na kusimamia ardhi ya kijiji.

**Cheti cha Ardhi ya Kijiji** kinakuwa badala ya Hatimiliki ya Ardhi ya Kijiji zilizotolewa kwa baadhi ya vijiji, ambazo zinapaswa kufutwa kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Vijiji ya 1999. Usimamizi wa ardhi ya kijiji ni pamoja na uwekaji na upimaji mipaka ya kijiji, upangaji kwa ushirikishwaji wa matumizi ya ardhi ya kijiji, ugawaji na umilikishaji wa maeneo ya ardhi kwa taasisi na watu binafsi (wanakijiji), kutoa Hatimiliki za haki za ardhi za kimila, na kuanzisha na kutunza Masjala ya Ardhi ya Kijiji, ambayo inapaswa kuwa sehemu ya Masjala ya Ardhi ya Wilaya.

### Utoaji wa Cheti cha Ardhi ya Kijiji

Cheti cha Ardhi ya Kijiji kinatolewa kwa jina la Rais, akikasimu mamlaka yake kwa Halmashauri ya Kijiji kusimamia Ardhi ya Kijiji. Cheti hiki kinahakikisha kukaliwa na kutumiwa kwa ardhi ya kijiji na wanakijiji kwa kuzingatia taratibu na kanuni za kimila zinazotumika katika ardhi ambako kijiji kipo. Cheti cha Ardhi ya Kijiji kinaandaliwa na Ofisa Ardhi wa Wilaya kwa kutumia Fomu ya Ardhi ya Vijiji Na. 16, kuwekewa mchoro wa mipaka ya kijiji na eneo lake, na kisha kusainiwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Kijiji na Afisa Mtendaji wa Kijiji, halafu kusajiliwa wilayani na kupewa namba ya usajili. Hatimaye Cheti hutumwa kwa Kamishna wa Ardhi kusainiwa na kuwekwa lakiri. Ofisi ya Kamishna hubaki na nakala moja kwa kumbukumbu, nakala mbili hutumwa kwa wilaya husika, ili nakala moja ibaki katika Masjala ya Ardhi ya Wilaya, nakala moja ipelekwe kwenye Masjala ya Ardhi ya Kijiji husika. Ni wajibu wa Halmashauri ya Kijiji kuangalia na kutunza kwa usalama Cheti cha Ardhi ya Kijiji. Inapotokea mipaka ya ardhi ya kijiji ikabadilishwa vyovyote vile, ni wajibu wa Halmashauri ya Kijiji kumjulisha mapema Kamishna wa Ardhi mabadiliko hayo. Vilevile Halmashauri ya Kijiji inapaswa imtumie Kamishna wa Ardhi Cheti cha Ardhi ya Kijiji, ili Kamishna afanye mabadiliko yaliyotokea katika cheti husika. Hii ina maana kuwa Kamishna wa Ardhi atatumia Daftari ya Ardhi za Vijiji.

### Kumbuka:

- (i) Yapo mambo mawili yanayowachanganya wananchi juu ya cheti cha ardhi ya kijiji na hatimiliki ya ardhi. leleweka kwamba, kabla ya ujio wa sheria za ardhi baadhi ya vijiji vilikuwa na hatimiliki za ardhi ya kijiji ambazo zilimilikishwa kwa halmashauri ya kijiji. Hii ina maana kuwa halmashauri ya kijiji ingeweza kutumia hati hiyo kama dhamana ya mkopo katika benki na ikishindwa kulipa ni sawa na wananchi wote wanaokaa katika ardhi hiyo wamewekwa rehani maana benki ikihitaji kulipwa mkopo wake ingeweza kuuza ardhi ambayo ndani yake kuna wananchi. Lakini kwa utaratibu wa cheti cha ardhi cha kijiji ina maana kila mwanakijiji anakuwa mmiliki wa ardhi na halmashauri kubakia kuwa msimamizi tu.
- (ii) Jambo la pili linalofanana ni hilo ni kwamba, endapo kijiji kilikuwa na hatimiliki ya aina hiyo, sheria za ardhi zinaibatilisha na kuwa haina maana tena maana kinachotambulika sasa ni cheti cha ardhi cha kijiji. Hata hivyo, cheti cha ardhi cha kijiji ni tofauti na cheti cha kijiji ambacho hutolewa kwa kila kijiji kilichosajiliwa rasmi na msajili wa vijiji katika wizara ya Tawala za mikoa na serikali za mitaa.

**Hatua ya nne:** Upangaji matumizi ya ardhi ya kijiji Kwa mujibu wa fungu la 33 la sheria ya mipango ya matumizi ya ardhi na fungu la 12 na la 13 la sheria ya ardhi ya vijiji, ardhi ya kijiji inagawanyika katika makundi matatu (3) kulingana na matumizi;

- (i) Ardhi inayokaliwa na kutumiwa na mtu, familia, au kikundi cha watu kwa mujibu wa sheria za kimila
- (ii) Ardhi ya makazi au matumizi ya jumuiya ambayo inaweza kutolewa kwa njia ya mgao na halmashauri ya kijiji
- (iii) Ardhi ya pamoja ambayo Halmashauri ya kijiji itapendekeza kwa mkutano mkuu wa kijiji maeneo na makusudio ya matumizi ya maeneo hayo.

Kwa kuzingatia Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Na. 6 ya 2007; Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya 1999, madhumuni ya kupanga ardhi ya vijiji ni pamoja na: Kutayarisha mpango wa usimamizi wa matumizi ya ardhi ya kijiji kwa kuzingatia matakwa ya umma na watu binafsi, kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi katika ardhi ya umma na ya watu binafsi, kukubaliana jinsi ya kutenga, kupima na kusajili ardhi ya huduma za jamii ardhi ya umma na ardhi ya watu binafsi na kuanzisha masjala ya ardhi ya kijiji. Pia, inawezekana kutunga sheria ndogo za kutekeleza makubaliano mbalimbali katika kijiji. Ili kuweza kufikia malengo hayo hapana budi mambo kadhaa ya awali yawe yametekelezwa kama vile;

- Kuwepo kwa Mpango wa Kazi wa Jamii (Community Action Plan-CAP) uliotayarishwa na wanakijiji wakati wa Tathmini ya Kijiji (PRA) kama ulivyoelezwa katika hatua za awali.
- Mipaka ya ardhi ya kijiji imewekwa /imepimwa, na inatambuliwa vizuri na jumuiya ya kijiji na vijiji jirani.
- Ramani ya msingi inayoonyesha matumizi ya ardhi yaliyopo.
- Uhamasikaji wa wanakijiji, Kamati husika ya ardhi, Halmashauri ya Kijiji, na wataalam.
- Upatikanaji wa rasimili na nyenzo.

Ikumbukwe kuwa mpango wa matumizi ya ardhi ya kijiji sharti uzingatie ugawaji wa ardhi katika matumizi haya: Makazi, Kilimo, Ufugaji (kuchungia), Misitu, vyanzo vya maji, wanyama pori, na matumizi mengine maalum k.m vile tambiko endapo ni sehemu ya matumizi na mahitaji ya wakazi wa maeneo husika. Kwa mfano;

- (i) Maeneo ya makazi; ni maeneo yaliyotengwa kwa ujenzi wa nyumba za kuishi na huduma mbalimbali za kijamii kama vile shule, zahanati, maofisi, huduma za maji, barabara, maduka, masoko, viwanja vya michezo, nyumba za ibada na makaburi.
- (ii) Maeneo ya kilimo; ni yale yanayotumika au yaliyotengwa kwa kulima mazao kulingana na aina ya mazao na mahitaji yake ya maji na huduma nyinginezo kama vile mazao ya kudumu, mazao ya msimu, mazao ya umwagiliaji, kilimo cha misitu
- (iii) Maeneo ya kuchungia; Nayo ni muhimu yakatengwa kwa kuzingatia mifumo ya ufugaji kama vile ufugaji huria, upatikanaji wa nyanda, malisho, nyika, njia za mifugo huduma za mifugo kama vile majosho na maji.
- (iv) Maeneo ya misitu; hasa endapo kuna maeneo yenye mimea asilia yenye miti mingi nayo yatengwe kulingana na usimamizi wake kuhusiana na uzalishaji yaani matumizi ya mbaao, mijengo, kuni, mkaa, asali, mitishamba, na uhifadhi wa mimea asilia.

Baada ya mpango wa matumizi ya ardhi kukamilika, halmashauri ya kijiji itatunga rasimu ya sheria ndogo ambayo itaratibu matumizi ya ardhi kama yalivyowekwa katika mpango wa matumizi ya kijiji. Kabla ya rasimu kupelekwa wilayani ni lazima viongozi wa vitongojia ama kamati ya maamuzi ya kijiji wawashirikishe wanavijiji katika maeneo yao juu ya malengo na madhumuni ya rasimu ya sheria ndogo. Sheria ndogo kabla ya kupitishwa na kutiwa sahihi na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya na Mkurugenzi wa Wilaya ni lazima ipitiwe ama na hakimu au mwanasheria wa Wilaya.

Halmashauri ya Kijiji kwa mujibu wa sheria ya ardhi ya kijiji ndiyo chombo chenye majukumu ya kusimamia ardhi ya kijiji kwa niaba ya wanakijiji wote. Usimamizi wa utekelezaji wa matumizi ya ardhi ya kijiji unafanywa na Halmashauri ya Kijiji kwa kushirikiana na wanakijiji pamoja na wadau wengine katika ngazi ya wilaya. Halmashauri ya kijiji husimamia ujenzi wa masjala ya kijiji ambayo hutunza nyaraka zote zikiwemo nakaza za hakimiliki za kimila ambazo hugawiwa kwa kila mwenye ardhi katika kijiji mara baada ya mchakato wa matumizi ya ardhi kufikia mwisho. Katika kurahisisha usimamizi wa ardhi ya kijiji inayomilikiwa kimila, ieleweke kwamba;

- (i) Mtu, familia au kundi la watu wanaweza kuomba hati ya haki ya ardhi ya kimila katika ardhi ya kijiji kwa halmashauri ya kijiji kwa kujaza fomu ya ardhi ya kijiji namba 18 ambayo italipiwa kwa kila ombi.

- (ii) Mwombaji anayekubaliwa hupewa barua ya toleo iliyosainiwa na Mwenyekiti na Afisa Mtendaji wa Kijiji yenye masharti ya eneo hilo.
- (iii) Mwombaji anapaswa kukubali au kukataabarua ya toleo katika muda wa siku 90 kwa maandishi kwa Halmashauri ya Kijiji.
- (iv) Halmashauri ya Kijiji ndani ya siku 90 baada ya kupokea kukubali kwa barua ya ahadi ya toleo itatoa hatimiliki ya haki ya ardhi ya kimila kwa mwombaji.

**Umilikaji ardhi kimila**

Huu ni utaratibu wa umilikaji ardhi kwa kufuata taratibu za kimila na desturi za jamii husika. Kila koo na jamii zilikuwa na taratibu zake za kupata, kutumia na kugawa ardhi ambazo zilikuwa zikitumika tangu enzi za mababu. Taratibu hizi zimeendelea kutambulika na kulindwa kisheria. Kabla ya Sheria namba 4 ya 1999 umiliki huu ulionekana ni wa hadhi ya chini kuliko ule wa Hati. Wakati wa ukoloni mahusiano kati ya mmiliki wa ardhi kimila na serikali ya kikoloni yalikuwa ni kati ya mtawala na mtawaliwa hayakuwa ya kisheria. Hivyo pale mkoloni alipohitaji ardhi aliweza kunyang'anya pasipo kutoa fidia. Hata hivyo, milki ya ardhi kimila hivi sasa inapewa hati ambayo inajulikana kama hatimiliki ya kimila na inaweza kupatikana kwa utaratibu ufuatao;

Kwanza, mipaka ya ardhi ya Kijiji inatakiwa iwe imebainishwa wakati wa kusajili kijiji. Cheti cha Kijiji hutolewa kwa kijiji husika ambacho kimesajiliwa kutokana na mchakato ulioelezwa hapo awali yaani wa kupata eneo la kiutawala kutokana na eneo hilo kutambuliwa na kuwekwa alama chini ya sheria yoyote au taratibu za kiutawala, makubaliano baina ya Halmashauri ya kijiji husika na vijiji jirani, au Kamishna wa ardhi (kwa ardhi ya kawaida), wasimamizi wa hifadhi (kwa ardhi ya hifadhi), mamlaka ya serikali za mitaa au mtu yoyote au chombo kinachokalia au kutumia ardhi kwa mujibu wa hakimiliki. Pili, kijiji kikishasajiliwa hupatiwa cheti cha ardhi ya kijiji. Kwa mujibu wa fungu la 7(7) hiki ni cheti kinachothibitisha mfumo wa ukajaji na utumiaji ardhi wa wanakijiji kwa mujibu wa sheria za kimila. Cheti hiki;

- (i) Hutolewa kwa amri ya Rais
- (ii) Kinaipa halmashauri ya kijiji majukumu ya kusimamia ardhi ya kijiji
- (iii) Kinabainisha mipaka ya Ardhi yakijiji badala ya hatimiliki zilizowahi kutolewa kwa baadhi ya halmashauri za vijiji.
- (iv) Kinathibitisha mamlaka ya ardhi halmashauri yakijiji kusimamia ardhi ya kijiji badala ya hatimiliki ambayo ambayo ingemaanisha halmashauri inamiliki ardhi ya kijiji hivyo kuwanyima wanakijiji kumiliki ardhi kwa mujibu wa sheria za sasa.
- (v) Endapo wanakijiji ni wafugaji au kwa kiasi kikubwa maisha yao yanategemea ufugaji, kitathibitisha matumizi ya ardhi kwajili ya malisho ya mifugo, ya ardhi isiyokuwa ya kijiji ambayo kwa desturi hutumika hivyo na watu hao.
- (vi) Endapo kijiji kimepata cheti halafu mipaka yake ikabadilika baada ya muda fulani kupita kijiji kitapaswa kuwasilisha taarifa hizi katika Halmashauri ya Wilaya hususani Idara ya Ardhi ili taratibu za ubadilishaji wa cheti uweze kufanyika.

Tatu, Kijiji kinapaswa kufanya mpango wa matumizi bora ya ardhi kulingana na mahitaji na vipaumbele vyao kupitia mkutano mkuu wa kijiji. Sheria ya mpango bora wa matumizi ya ardhi, namba 6 ya mwaka 2007 ndiyo sheria inayotoa mwongozo katika hatua hii.

Nne, baada ya mchakato wa uandaaji wa cheti cha ardhi ya kijiji na mpango wa matumizi bora ya ardhi ya kijiji kukamilika, ni fursa kwa kila mwanakijiji kupewa Cheti cha hakimiliki ya kimila ambacho maandalizi na upatikanaji wake vimefafanuliwa hapa chini kwa undani.

**Cheti cha hakimiliki ya kimila**

Hiki ni cheti kinachotolewa na halmashauri ya kijiji kwa mujibu wa fungu la 25 la sheria ya ardhi ya vijiji Na. 5 ya mwaka 1999 ili kutambua au kuthibitisha umiliki wa ardhi wa mwombaji kwa taratibu za kimila (reja katika vifungu 23, 24). Fungu la 25 linazungumzia cheti hiki kuwa:-

- Kitatolewa katika fomu iliyoainishwa (namba 21 kwa mujibu kanuni ya sheria ya ardhi ya Kijiji),

- Kitatiwa saina na mwenyekiti pamoja na Afisa mtendaji wa halmashauri ya kijiji,
- Kitatiwa saina au kuwekwa alama na mtu ambaye atapewa hakimiliki ya kimila inayohusika chini ya ukurasa wa cheti hicho,
- Kitatiwa saina, kuwekwa lakiri na kusajiliwa na afisa ardhi wa wilaya ambamo kijiji hicho kimo,
- Inaweza kutolewa kwa kipindi kisicho na kikomo au kwa kipindi chochote ambacho ni pungufu (fungu la 27),
- Italiwiwa kodi ya pango na wageni au wasio wenyeji wa kawaida (reja vifungu 28, 22(2) pamoja na taasisi isiyo ya kijiji.

Kwa mujibu wa fungu la 29, kila hatimiliki itatolewa kwa masharti yaliyoainishwa katika fungu hilo na mengineyo yatakawekwa. Mmiliki atahakikisha kuwa

- Ataitumia ardhi hiyo.
- Ahakikishe wanaotumia ardhi kwa idhini yake wanaitunza na kuidumisha ardhi hiyo katika hali nzuri.
- Kama inatumika kwa kilimo ilimwe kwa kuzingatia desturi nzuri za kilimo.
- Wafugaji kutumia ardhi kwa namna endelevu kwa kutumia utaalamu wa eneo husika.
- Mmiliki atalipa kodi, ghrama na ushuru na malipo mengine yanayostahili.
- Ataendelea kuishi katika kijiji hicho.

Wakati suala la kila kijiji kuwa na cheti cha ardhi cha kijiji na hatimaye kuwezesha wakazi wake kuwa na hakimiliki za kimila linaonekana kuwa ni la kimapinduzi na kimaendeleo, ni vema pia ikasisitizwa kuwa utaratibu mzima wa kuvipata vyeti hivyo unahusisha gharama na mlolongo mrefu hadi kuweza kuvipata vyeti hivyo ikiwa ni pamoja na mchakato wa mpango wa matumizi bora ya ardhi katika kijiji husika. Katika sura ya tatu ya kitini hiki masuala yanayohusu mpango wa matumizi bora ya ardhi yatajadiliwa kwa kina.

**Hatua ya sita: Usimamizi wa ardhi na uimarishaji**

Baada ya mpango wa matumizi ya ardhi kukamilika serikali ya kijiji inatakiwa kusimamia sheria ndogo kwa kushirikiana na kamati ambayo itakuwa imeundwa mahususi kwa kusimamia matumizi ya ardhi. Maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kilimo, kuchungia mifugo, misitu, wanyama pori na makazi yanatakiwa kuheshimiwa na kutumiwa kama yaliyopangwa ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima.

Kama mpango wa matumizi ya ardhi utaheshimiwa wanakijiji wanafaidika na rasilimali zao na kuendelea sasa. Serikali ya kijiji inatakiwa idumishe mahusiano na timu ya PLUM ya wilaya katika masuala ya ushauri juu ya masuala ya kitaalamu na kiufundi. Mabadiliko mengine ya matumizi na umiliki yanatakiwa yafanyike kwa utaratibu uliowekwa na sheria ndogo au Sheria ya Ardhi ya Vijiji.

**Hitimisho la mada**

Kama ilivyoelezwa kwa ufasaha katika mada hii, mhimili mkuu wa uandaaji wa mpango wa matumizi ya ardhi ya kijiji wenye ufanisi ni ushiriki wa wananchi wenyewe hatua kwa hatua. Zipo hatua ambazo wananchi wanashiriki moja kwa moja na zipo hatua ambazo wanashiriki kupitia uwakilishi wao. Hatua zote ni muhimu na ni vema wananchi wakajitokeza kuwa sehemu ya uamuzi huu wa msingi kuhusiana na ardhi wanayoitegemea kwa maisha yao. Jambo la pili na la muhimu pia, ni jinsi ambavyo mpango wa matumizi ya ardhi ya kijiji unavyoweza kutoa suluhu kwa matatizo sugu ya migogoro ya mipaka kati na baina ya wanavijiji, kukabiliana na uharibifu wa mazingira na hata kuchangia katika jitihada za kukabili athari mbaya za mabadiliko ya tabia nchi. Hii inatokana na ukweli kuwa, matumizi ya ardhi yaliyopangwa yanasaidia hifadhi ya mazingira na matumizi endelevu ya rasilimali ambazo zinahitajika kwa kizazi cha sasa na cha baadae.